# Ramani ya Familia

## Karibu kwenye Ramani ya Familia

Unaweza kutazama video ili kujifunza zaidi kuhusu ramani hii.

## Haki Zako za Elimu

Nchini Marekani, shule na familia hufanya kazi pamoja ili kuwasaidia watoto kujifunza na kukua. Kuna sheria za kuhakikisha kwamba kila mtoto anapata elimu bora. Haki na ulinzi uleule wa shule za umma hutumika kwa wanafunzi na familia zote. Wanafunzi wanaojifunza Kiingereza kama lugha mpya wana ulinzi unaohusiana na kupokea misaada ya lugha na kuweza kushiriki katika shughuli zote za shule.

Familia zinapaswa kuelewa haki za wanafunzi wao. Kisha, watambue wanachotarajia kutoka kwa shule yao. Wanaweza kuhakikisha kwamba wanapata elimu bora iwezekanavyo. Hili husaidia kuwatayarisha wanafunzi kwa ajili ya wakati ujao mwangavu.

Jifunze zaidi kuhusu haki za elimu.

## Machaguo ya Shule

Rasilimali hii itakusaidia kujifunza kuhusu machaguo mbalimbali ya shule yanayopatikana kwa ajili yako na familia yako katika jimbo la Ohio. Inajumuisha habari kuhusu shule za jadi za umma, shule za mkataba, na shule za kibinafsi. Kuna sababu nyingi kwa nini familia huchagua aina moja ya shule badala ya nyingine. Ohio ina machaguo manane ya shule pamoja na machaguo kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu.

Watoto wana uwezekano mkubwa wa kufanya vizuri shuleni wakati wazazi au walezi wao wanahusishwa. Ili kuhusishwa katika elimu ya mtoto wao, ni muhimu kwa wazazi au walezi kuelewa jinsi shule zinavyopangwa. Mifumo ya shule inaweza kuwa tofauti. Inasaidia kujua ni machaguo gani familia, wazazi, au walezi waliyo nayo ya kumsaidia mtoto wao.

[Copyright] ©2024 Kituo cha Elimu na Mafunzo ya Ajira (CETE), The Ohio State University

Tembelea Chagua Kifaa cha Shule katika Kituo cha Ushirikiano wa Familia cha Jimbo Zima la Ohio ili kuisaidia familia yako kufanya uchaguzi bora zaidi wa shule kwa ajili ya mtoto wako.

# Uandikishaji

## Kumwandikisha Mtoto Wako Ohio

Kuanza shule mpya ni wakati wa kusisimua kwa watoto na familia zao. Ni mwanzo wa mahusiano mapya na marafiki na walimu. Pia ni wakati ambapo familia yako inakuwa sehemu ya jamii ya shule. Kabla watoto wako waweze kuanza shule, ni lazima uwaandikishe. Wakati wa uandikishaji, utajifunza kuhusu programu nyingi na kile shule inaandaa kwa wanafunzi na familia.

Jifunze zaidi kuhusu kumwandikisha mtoto wako shuleni.

## Kuelewa Hudhurio la Shule

Watoto wanaoenda shuleni mara nyingi wana uwezekano mkubwa wa kufanya vizuri shuleni. Wanafunzi wanaohudhuria shule kila siku wanaweza mara tisa zaidi kuhitimu shule ya upili. Pia wanaweza mara sita zaidi kufikia mafanikio ya kusoma wanapofika darasa la tatu. Kwa sababu hii, watoto wanatarajiwa kuhudhuria shule kwa ukawaida iwezekanavyo. Katika Ohio, shule huweka rekodi ya idadi ya saa ambazo watoto huhudhuria shule.

Jifunze zaidi kuhusu hudhurio la shule.

## Kuelewa Maendeleo ya Kitaaluma ya Mtoto Wako

Kuelewa maendeleo ya kitaaluma ya mtoto wako ni muhimu kwa mafanikio yake shuleni. Kwa kujua jinsi anavyofanya vizuri katika masomo yake, unaweza kumsaidia na kumwongoza kwa mafanikio. Kuna njia mbalimbali ambazo shule ya mtoto wako inaweza kutathmini masomo yake, kama vile mitihani na kazi. Hizi huandaa uelewaji muhimu wa safari yake ya elimu.

Jifunze zaidi kuhusu maendeleo ya kitaaluma na kutuza alama.

[Copyright] ©2024 Kituo cha Elimu na Mafunzo ya Ajira (CETE), The Ohio State University 

## Misaada ya Lugha ya Kiingereza

Shule na waelimishaji wa Ohio wanawataka watoto watumie fursa ili waweze kuwasiliana vizuri ulimwenguni. Hii ni pamoja na kuandaa misaada ya lugha ya Kiingereza kwa wanafunzi wanaoihitaji. Shule zina hatua na misaada hususa ya kuwasaidia wanafunzi kuboresha ustadi wao wa Kiingereza.

Jifunze zaidi kuhusu misaada ya lugha ya Kiingereza.

## Kufanya Kazi Pamoja kwa Ajili ya Mafanikio

### Kufanya Kazi Pamoja na Shule kwa Ajili ya Mafanikio ya Mtoto Wako

Hakuna mtu anayemjua mtoto wako vizuri kuliko wewe na familia yako. Unaweza kuwasiliana na shule unapotaka kujifunza kuhusu jinsi ya kutegemeza elimu ya mtoto wako au mtoto wako anapohitaji msaada. Unaweza pia kuwasiliana na shule ili kuhakikisha kwamba mtoto wako anaendelea vizuri.

Jifunze zaidi kuhusu kufanya kazi na shule.

### Jinsi ya Kushiriki Katika Kamati na Timu za Shule

Familia na walimu wanapofanya kazi pamoja, watoto wana uwezekano mkubwa wa kufanikiwa, kuhudhuria shule kila siku, na kuhisi wameunganishwa na wanafunzi wenzao na walimu. Wazazi na walezi wanaohusika na shule hujihisi kuwa sehemu ya jamii ya shule. Njia moja muhimu ambayo familia fulani huchagua kushiriki katika shule ya mtoto wao ni kwa kujiunga na timu au kamati ya shule. Wazazi na walezi wanaweza kukutana na familia nyingine na kufanya kazi na walimu na wasimamizi ili kufanya maamuzi kuhusu shule au wilaya.

Jifunze zaidi kuhusu kushiriki katika shule ya mtoto wako.

## Kuhitimu

"Tunajua si rahisi, lakini mnafanya kazi nzuri kwa ajili ya wakati ujao wa watoto wenu." – Mwalimu wa Ohio

[Copyright] ©2024 Kituo cha Elimu na Mafunzo ya Ajira (CETE), The Ohio State University 

## Kutegemeza Kuhitimu kwa Mtoto Wako

Kuhitimu shule ya sekondari ni hatua muhimu ya kwanza kwa watu wazima vijana katika kuchunguza machaguo yao ya chuo na kazi. Ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wako tayari kwa ajili ya mafanikio ya baadaye, shule za Ohio zina matakwa ambayo lazima wanafunzi wakamilishe ili kuhitimu. Unaweza kumsaidia mtoto wako ahitimu na ajitayarishe kwa ajili ya maisha yake ya baadaye. Kagua matakwa ya kuhitimu na njia mbalimbali ambazo unaweza kuyaunga mkono.

Jifunze zaidi kuhusu kuhitimu.

## Kumwandaa Mtoto Wako kwa Ajili ya Wakati Ujao Mwangavu

Familia yako ina jukumu muhimu katika kumwandaa mtoto wako kwa ajili ya wakati ujao. Haijalishi ni njia gani mtoto wako anachukua, unaweza kumtegemeza kwa kumsaidia kuchunguza machaguo yake kwa ajili ya wakati ujao. Unaweza kumwuliza kuhusu njia au kazi wanazovutiwa nazo. Au unaweza kuanza kwa kumwuliza kuhusu ndoto na malengo yake. Unaweza pia kuchunguza ni msaada gani unaopatikana katika shule ya mtoto wako na katika jamii yako.

Jifunze zaidi kuhusu machaguo ya chuo na kazi.

# Misaada ya Ziada

## Kumsaidia Mtoto Wako na Masomo ya Mtandaoni (au Intaneti)

Masomo ya mtandaoni ni njia ya kujifunza kwa kutumia teknolojia na imebadilisha njia tunayojifunza shuleni. Inawapa watoto wa umri wote fursa ya kukuza haraka uelewaji wao wa ulimwengu unaowazunguka. Ili kupata faida kamili za teknolojia hii, shule hutumia masomo ya mtandaoni ili kuwasaidia wanafunzi na masomo yao. Njia ambayo shule hutumia masomo ya mtandaoni inaweza kuwa tofauti katika kila shule na darasa. Ni muhimu kuelewa jinsi ya kutegemeza masomo ya mtandaoni nyumbani.

Jifunze zaidi kuhusu masomo ya mtandaoni

## Programu kwa Wanafunzi Nje ya Muda wa Shule

Katika Ohio, kuna programu ambazo wanafunzi wanaweza kujiunga nazo nje ya muda

wa shule. Programu hizi zinaweza kuwa kabla au baada ya shule. Nyingine zinaweza kuwa wakati wa mapumziko ya shule. Programu fulani zinaweza kuandaa msaada wa ziada kwa wanafunzi wanaohitaji msaada na shule. Zinaweza kuwasaidia watoto kufanya vizuri zaidi shuleni kwa kuwapa mahali patulivu pa kufanyia kazi za nyumbani na kufikia kompyuta na intaneti. Zinaweza pia kuandaa msaada wa ziada na kazi za shule au kufanya shughuli za kufurahisha zinazofundisha mambo mapya. Katika programu hizi, watoto wanaweza kupata marafiki wapya na kujifunza kutoka kwa wengine. Huenda familia zikahitaji kumsajili mtoto wao au kufikia sheria fulani. Programu hizi zinaweza kuwa bila malipo au kunaweza kuwa na gharama za ziada. Wengine hata huwapatia watoto chakula au msaada wa usafiri.

Jifunze zaidi kuhusu programu za nje ya shule.

### Kutegemeza Afya ya Akili ya Mtoto Wako

Katika Ohio, shule hufanya kazi ili kumtegemeza mtoto mzima. Hili linamaanisha kwamba shule zinajali kuhusu mafanikio ya kitaaluma na ustawi wa kila mwanafunzi. Kwa sababu hii, shule huandaa rasilimali za kusaidia afya ya akili ya wanafunzi.

Jifunze zaidi kuhusu kutegemeza afya ya akili ya mtoto wako.

### Kutumia Wakalimani kwa Ajili ya Mawasiliano na Shule

Katika Ohio, shule na familia hufanya kazi pamoja ili kuwasaidia watoto wafanikiwe. Wanafanya hivi kwa kuzungumza na kushiriki habari muhimu na kila mmoja wao. Shule lazima zishiriki habari katika lugha ambazo familia zinapendelea. Familia yako inaweza kupata msaada kutoka kwa wakalimani katika kuuliza maswali na kushiriki mawazo au mahangaiko yako na shule.

Jifunze zaidi kuhusu kutumia wakalimani.

## Orodha ya Mashirika

### Rasilimali katika Ohio

Mashirika haya yanalenga kuzisaidia familia zilizo mpya katika Ohio na zinazozungumza lugha nyingine isipokuwa Kiingereza.

Pakua nakala ya orodha ya mashirika kwenye kompyuta au kifaa chako.

## Kamusi

Kamusi hii imeundwa ili kukuandalia ufafanuzi na maelezo rahisi ya maneno ya kawaida kuhusu shule na elimu. Kifaa hiki kitakusaidia kuelewa vizuri zaidi elimu ya mtoto wako.

Chunguza kamusi hii.

*Vifaa hivi vinalenga kuimarisha ustawi wa kitaaluma, wanafunzi na matokeo ya chuo na kazi kwa wanafunzi wa lugha nyingi wa Ohio. Rasilimali ziliundwa kupitia juhudi ya pamoja kati ya Idara ya Elimu na Kazi ya Ohio (ODEW) na Kituo cha The Ohio State University cha Elimu na Mafunzo ya Ajira (CETE) pamoja na kikundi kilichojitolea cha watetezi wa familia, viongozi wa jamii, wafanyakazi wa wilaya ya shule, na walimu.*

[Copyright] ©2024 Kituo cha Elimu na Mafunzo ya Ajira (CETE), The Ohio State University